# Sheria ya Ulinzi wa Kimataifa, 2015.

**[Taarifa itatolewa chini ya sehemu ya 70(10)(a) ya Sheria ya Ulinzi wa Kimataifa, 2015]**

## Muhtasari wa maelezo - Mipango ya Mpito

## Utangulizi wa UTARATIBU WA KUTUMA OMBI MOJA kwa ajili ya uchunguzi na uamuzi wa maombi ya Ulinzi wa Kimataifa (Hadhi ya Ukimbizi na Hifadhi Mbadala) na Kibali cha Kusalia

**Taarifa hii ni ya maelezo na mwongozo tu. Si ushauri wa kisheria na haikusudii kutoa tafsiri ya kisheria ya Sheria ya Ulinzi wa Kimataifa 2015. Muhtasari huu wa maelezo unashughulikia tu kategoria kuu za kesi ambazo zinaathiriwa na matoleo ya mpito ya Sheria ya Ulinzi wa Kimataifa, 2015. Hayashughulikii hali zote zinazowezekana ambapo matoleo ya mpito yanaweza kutumika. Kama unahitaji maelezo zaidi kuhusu Sheria ya 2015 na matoleo yake kuhusu kesi yako, unastahili kutafuta ushauri wa kisheria.**

**Muhtasari huu wa maelezo unastahili kusomwa pamoja na Kijitabu cha kando cha Maelezo kwa Waombaji wa Ulinzi wa Kimataifa (IPO 1) na Dodoso ya Ulinzi wa Kimataifa (IPO 2) ambacho kimeambatishwa.**

## 1. Utangulizi

1.1 Sheria ya Ulinzi wa Kimataifa, 2015 (sheria ya 2015) ilianzishwa na Waziri wa Haki na Usawa (“Waziri”) mnamo tarehe **31 Desemba 2016**. Katika Muhtasari huu wa maelezo, hii inarejelewa kama "tarehe ya kuanza".

1.2 Muhtasari huu wa maelezo unakupa maelezo ya mipango ya mpito yanayosimamia uchunguzi na uamuzi waa maombi (katika awamu nyingine za mchakato huu) ya ulinzi wa kimataifa (hadhi ya ukimbizi na hifadhi mbadala) chini ya Sheria ya Ulinzi

wa Kimataifa, 2015 ambayo yaliwasilishwa Nchini (Ayalandi) kabla ya tarehe ya kuanza. Yanakupa pia maelezo mengine yanayohusiana na kibali cha kusalia.

1.3 Yanakusudia kukusaidia kuelewa mipangilio ya kutumia katika kuhamisha

- maombi mengine ya hadhi ya ukimbizi na hifadhi mbadala kutoka kwa Ofisi ya Kamishna wa Maombi ya Ukimbizi (ORAC) na
- maombi mengine ya rufaa ya ukimbizi kutoka kwa Mahakama ya Rufaa ya Wakimbizi (RAT)

ambayo yaliwasilishwa kabla ya tarehe 31 Desemba 2016, kwa Ofisi ya Ulinzi wa Kimataifa ya Huduma ya Uraia na Uhamiaji ya Ayalandi kwa ajili ya ukamilishaji wa mchakato chini ya Sheria ya 2015.

1.4 Maelezo zaidi ya kina kuhusu misingi ambayo mtu ana haki ya kupata hadhi ya ukimbizi au hifadhi mbadala na taratibu za kuomba katika Ofisi ya Ulinzi wa Kimataifa (IPO) yameelezewa katika Kijitabu kilichoambatishwa cha maelezo ya Waombaji wa Ulinzi wa Kimataifa (IPO 1). Kijitabu hiki kinaelezea pia haki na majukumu yako ni yapi kama mwomba ulinzi wa kimataifa na utakuwa ukihusika na nani wakati wa mchakato huu wa maombi. Kijitabu hiki pia kinaelezea taratibu ambazo zinatumiwa na Waziri ili kupata kibali cha kusalia kwa misingi tofauti kando na hitaji la ulinzi wa kimataifa.

1.5 Tumeambatisha pia Maombi ya Dodoso ya Ulinzi wa Kimataifa (IPO 2).

1.6 Ni muhimu na ni ya manufaa kwako kusoma Muhtasari huu wa maelezo na Kijitabu kilichoambatishwa cha maelezo na Dodoso kwa makini na utafute ushauri wa kisheria kama inavyohitajika ili uweze kuunga mkono maombi yako na **uhakikishe kuwa unaelewa jinsi mipango ya mpito ya Sheria ya 2015 inatumika kwako.**

## 2. Lengo la Sheria ya Ulinzi wa Kimataifa ya 2015

2.1 Sheria ya 2015 inawezesha utangulizi wa utaratibu wa kutuma ombi moja ambalo linawezesha misingi yote ya kutafuta ulinzi wa kimataifa (hadhi ya ukimbizi na hifadhi

mbadala) na kibali cha kusalia Nchini kwa sababu nyingine ambazo zitachunguzwa na kubainishwa katika mchakato mmoja mfululizo.

2.2 Sheria ya 2015 ina mipango ya mpito ambayo inatumika katika maombi mengine ya hadhi ya ukimbizi na hifadhi mbadala ambayo yaliwasilishwa kabla ya tarehe ya kuanza (**angalia sehemu ya 4**)

## 3. Je, ni nani atakayeamua maombi na rufaa chini ya Sheria ya 2015?

3.1 Chini ya Sheria ya 2015, ORAC imeondolewa. Jukumu la uchunguzi na uamuzi wa masuala ya maombi ya ulinzi wa kimataifa na kibali husika cha kusalia nchini yaliyoshughulikiwa katika Muhtasari huu wa maelezo yamehamishwa hadi Ofisi ya Ulinzi wa Kimataifa (IPO) ya Huduma ya Uraia na Uhamiaji ya Ayalandi (INIS) tangu tarehe ya kuanza na kulingana na matoleo ya Sheria ya 2015.

3.2 Chini ya Sheria ya 2015, RAT pia imeondolewa. Jukumu la uamuzi wa rufaa ya maombi ya ulinzi wa kimataifa limehamishwa hadi Mahakama ya Rufaa ya Ulinzi wa Kimataifa (IPAT) tangu tarehe ya kuanza na kulingana na matoleo ya Sheria ya 2015.

## 4. Mipango ya mpito ya maombi <u>yaliyopo</u> ya hadhi ya ukimbizi na hifadhi mbadala ambayo hayajakamilishwa kabla ya tarehe ya kuanza

4.1 Isipokuwa maombi hayo yanastahili kushughulikiwa chini ya Kanuni za EU Dublin, ambapo mipango mingine ya kando itatumika (angalia <u>sehemu</u> ya 10 ya Kijitabu cha Maelezo kwa Waombaji wa Ulinzi wa Kimataifa), mipango ifuatayo ya mpito itatumika kwa maombi ya hadhi ya ukimbizi na hifadhi mbadala yaliyowasilishwa kabla ya tarehe ya kuanza na ambayo hayakukamilishwa tarehe hiyo.

**Kategoria ya 1 - Maombi ya ukimbizi katika ORAC**
Kama uliomba hadhi ya ukimbizi kabla ya tarehe ya kuanza lakini ripoti haikuwa imeandaliwa na ORAC chini ya sehemu ya 13 ya Sheria ya Wakambizi ya 1996 kabla ya tarehe hiyo (kwa maneno mengine, pendekezo halikutolewa), maombi yako yatachukuliwa kuwa maombi ya ulinzi wa kimataifa (ya hadhi ya ukimbizi na hifadhi

mbadala) chini ya Sheria ya 2015. Faili yako imehamishwa kwa Ofisi ya Ulinzi wa Kimataifa ili kuzingatiwa kama una haki ya hadhi ya ukimbizi au ya hifadhi mbadala au la.

Kama utachukuliwa kuwa hustahili hadhi ya ukimbizi au ya hifadhi mbadala, Waziri mara moja atafikiria kama unastahili kupewa kibali cha kusalia kwa sababu nyingine. Uamuzi huu utategemea hati zote ambazo umewasilisha tayari na hutaulizwa utume maombi mapya ya kibali cha kusalia.

**Kategoria ya 2 - Maombi ya rufaa ya ukimbizi**

Kama maombi yako ya hadhi ya ukimbizi yalikuwa ya rufaa kwa RAT kabla ya tarehe ya kuanza lakini hayakuwa yameamuliwa na RAT kabla ya tarehe hiyo, utachukuliwa kuwa umeomba ulinzi wa kimataifa chini ya Sheria ya 2015. Faili yako imehamishwa kwa IPO ili kuzingatiwa kama una haki ya hifadhi mbadala pekee. Katika hali hizo, pendekezo la maombi ya hadhi yako ya ukimbizi lililofanywa na ORAC litahifadhiwa na litaendelea kutumika. Kama IPO itapendekeza kuwa hustahili kupewa hifadhi mbadala, Waziri mara moja atafikiria kama unastahili kupewa kibali cha kusalia kwa sababu nyingine. Rufaa ya hapo awali iliyotumwa kwa RAT itahifadhiwa na kuhamishwa kwa IPAT mpya. Ukinyimwa hifadhi mbadala, unaweza pia kukata rufaa ya pendekezo la hifadhi mbadala la IPO kwa IPAT na maombi hayo mawili ya rufaa yatashughulikiwa kama moja na kusikilizwa pamoja. Ukinyimwa pia kibali cha kusalia na IPO, unastahili kukumbuka kuwa chini ya Sheria ya 2015 huwezi kukata rufaa ya uamuzi wa kibali cha kusalia kwa IPAT.

**Kategoria ya 3 - Hifadhi Mbadala**

Kama umeomba hifadhi mbadala kabla ya tarehe ya kuanza na ORAC haijaanzisha uchunguzi wake kabla ya tarehe hiyo, maombi yako yatachukuliwa kuwa ni maombi ya ulinzi wa kimataifa chini ya Sheria ya 2015. Faili yako imehamishwa kwa IPO ili kuzingatiwa kama una haki ya masuala yoyote ya hifadhi mbadala pekee. Katika hali hiyo, pendekezo la maombi yako ya hadhi ya ukimbizi lililofanywa na ORAC (au uamuzi

wa RAT kuhusu maombi ya rufaa, kama upo) litahifadhiwa na kuendelea kutumika.

**Maelezo mengine**

(i) Kama uliomba hifadhi mbadala kabla ya tarehe ya kuanza na ORAC ilikuwa imeanza uchunguzi wa maombi kabla ya tarehe hiyo, maombi hayo hayataathiriwa na Sheria ya 2015, licha ya kweli kuwa IPO itachukua shughuli zote za ORAC. Sheria zilizopo zitaendelea kutumika na IPO itachunguza maombi yako chini ya taratibu za zamani.

(ii) Kama umetuma maombi ya hifadhi mbadala na maombi haya yamekatiwa rufaa mbele ya RAT kabla ya tarehe ya kuanza, maombi hayo ya rufaa yatahamishwa kwa IPAT ambayo itayaamua chini ya sheria zilizopo.

## 5. Kibali cha Kusalia

5.1 Iwapo IPO itapendekeza kuwa maombi yako ya ulinzi wa kimataifa chini ya Sheria ya 2015 (iwe kuhusu hadhi ya ukimbizi na hifadhi mbadala au hifadhi mbadala pekee), uamuzi utafanywa kuhusu kama unastahili kupewa kibali cha kusalia Nchini kwa sababu nyingine.

5.2 Ni muhimu kukumbuka kuwa taratibu zimebadilika kulingana na Sheria ya 2015, sasa Waziri hatakuandikia tena akikualika ujieleze kwa nini unastahili kupewa kibali cha kusalia Nchini. Badala yake, hii itazingatiwa na IPO iwapo itapendekeza kuwa maombi yako ya ulinzi wa kimataifa yakataliwa. Uamuzi utatolewa kulingana na maelezo na hati zilizotolewa tayari katika kesi yako.

5.3 Kwa hivyo, kama kesi yako imehamishwa hadi kwa IPO ili kuchukuliwa kama maombi ya ulinzi wa kimataifa chini ya Sheria ya 2015, lazima ueleze kwa kuandika sababu zozote za kwanini unaonelea unastahili kupewa kibali cha kusalia katika sehemu inayofaa ya Maombi ya Dodoso ya Ulinzi wa Kimataifa (IPO 2). Kwa mfano, hali zako za kifamilia na kinyumbani, hali ya uhusiano wako na Serikali, tabia na maadili yako ndani na

nje ya Nchi na sababu za kiufadhili ambazo zote ni masuala muhimu. Kwa ufafanuzi kamili wa masuala muhimu, tafadhali angalia Kijitabu cha Maelezo kwa Waombaji wa Ulinzi wa Kimataifa (IPO 1).

5.4 Unastahili pia kufahamisha IPO (kwa niaba ya Waziri) kuhusu mabadiliko yoyote ambayo yanaweza kuwa muhimu katika hali zako (k.m. hali zako za kifamilia au kinyumbani au hali katika nchi yako ya asili).

## 6. Kama nimeshughulikiwa na mipango ya mpito, ninastahili kutuma maombi mengine ya ulinzi wa kimataifa?

6.1 Kama maombi yako ya ulinzi wa kimataifa yako kati ya kategoria zilizotajwa katika sehemu ya 4 hapa juu, **hustahili** kutuma maombi mapya ya ulinzi wa kimataifa kwa Waziri lakini unastahili ufuate maagizo katika sehemu ya 7 hapa chini yanayohusu ukamilishaji wa sehemu muhimu za Maombi ya Dodoso ya Ulinzi wa Kimataifa (IPO 2).

## 7. Ukamilishaji wa Maombi ya Dodoso ya Ulinzi wa Kimataifa

7.1 Kama maombi yako yamechukuliwa kuwa ni maombi ya ulinzi wa kimataifa chini ya Kategoria 1, 2, au 3 zilizoelezwa katika sehemu ya 4 hapa juu, unastahili kukamilisha Maombi ya Dodoso ya Ulinzi wa Kimataifa kama ifuatavyo:

**Kesi za Kategoria ya 1 (hadhi ya ukimbizi, hifadhi mbadala na kibali cha kusalia)**
Tafadhali kamilisha Dososo **kwa ukamilifu.**

**Kesi za Kategoria ya 2 (hifadhi mbadala na kibali cha kusalia)**

Tafadhali kamilisha Dodoso lakini usikamilishe sehemu inayohusu hadhi ya ukimbizi **(Maswali ya 63a na 63b).**

**Kesi za Kategoria ya 3 (hifadhi mbadala na kibali cha kusalia)**

Tafadhali kamilisha Dodoso lakini usikamilishe sehemu inayohusu hadhi ya ukimbizi **(Maswali ya 63a na 63b).**

7.2 Pia una haki ya kutoa maelezo yoyote ya ziada kwa **kuandika barua** inayounga mkono maombi yako ya ulinzi wa kimataifa ambayo unaona inafaa. Si lazima uwasilishe tena hati zozote ambazo umewasilisha tayari zinazohusiana na maombi yako kwa kuwa hati hizo zote zitasalia kwenye faili yako.

7.3 Unastahili kurejesha Maombi ya Dodoso ya Ulinzi wa Kimataifa (IPO 2) pamoja na maelezo yoyote ya ziada ambayo unayategemea yanayounga mkono maombi yako ya ulinzi wa kimataifa na ya kibali cha kusalia (ikiwa yapo), ikiwezekana **kabla ya siku 20 za kufanya kazi** kuanzia tarehe uliyopokea barua pamoja na Muhtasari huu wa maelezo ndani ya bahasha iliyoambatishwa ya FREEPOST kwa

**Transitional Cases Section,**
**International Protection Office,**
**Irish Naturalisation and Immigration Service,**
**79 - 83 Lower Mount Street,**
**Dublin 2,**
**D02 ND99**

7.4 **Ikiwa wewe na/au mshauri wako wa kisheria mnahitaji kutoa maelezo ya ziada kwa IPO baada ya kuwasilisha maelezo katika aya ya 7.3 hapa juu, unastahili kufanya hivyo haraka iwezekanavyo na, kama unaweza kufanya hivyo, usipitishe wiki mbili kabla ya tarehe ya mahojiano yako yaliyopangwa. Muda huu utawezesha tafsiri ya hati kama itahitajika na kuhakikisha kuwa mhojaji wa IPO ana karatasi zote zinazopatikana na kuzingatiwa mapema kabla ya tarehe ya mahojiano.**

## 8. Je, ni lini nitahojiwa chini ya Sheria ya Ulinzi wa Kimataifa ya 2015?

8.1 Ukikamilisha na urejeshe Maombi yako ya Dodoso ya Ulinzi wa Kimataifa (IPO 2) na maelezo yoyote ya ziada kulingana na sehemu ya 7, Ofisi ya Ulinzi wa Kimataifa itawasiliana na wewe kwa wakati unaofaa kuhusu mipango ya mahojiano yako kama yatahitajika. Huenda mahojiano yako yasipangwe kwa miezi kadhaa kwa sababu ya idadi kubwa ya maombi ya kuchakatwa na IPO.

8.2 **Hakuna** haja ya kuwasiliana na Ofisi ya Ulinzi wa Kimataifa moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja ili kuomba mahojiano.

**9. Ni lini maombi yangu ya rufaa yatasikilizwa na IPAT?**

9.1 Kama una maombi yanayosubiri ya rufaa ya ukimbizi ambayo hayakuamuliwa kabla ya tarehe ya kuanza, faili yako itahamishwa kwa IPO kama ilivyoelezwa katika sehemu ya 4, hapa juu.

9.2 Kama una maombi ya rufaa yanayosubiri ya hifadhi mbadala, yatasikilizwa na IPAT na utafahamishwa kuhusu siku ya kusikilizwa na IPAT.

**10. Habari Zaidi**

10.1 Maswali yoyote yanayohusu yaliyomo katika Muhtasari huu wa maelezo yanastahili kuelekezwa **kwa kuandika barua** kwa Customer Service Centre, International Protection Office, Irish Naturalisation and Immigration Service, 79-83 Lower Mount Street, Dublin 2 au kwa **info@ipo.gov.ie**

10.2 Sheria ya Ulinzi wa Kimataifa ya 2015 na Sheria nyingine Husika zinaweza kupatikana kikamilifu katika **www.ipo.gov.ie**

10.3 Muhtasari huu wa maelezo unapatikana pia kwa lugha mbalimbali kwenye anwani ya barua pepe iliyo hapa juu.

10.4 Unaweza kupata huduma za Bodi ya Usaidizi wa Kisheria kuhusiana na maombi yako ya ulinzi wa kimataifa au kibali cha kusalia. Vingenevyo, unaweza kushauriana na wakili wa kibinafsi kwa gharama yako ili akusaidie.

10.5 Pia una haki ya kushauriana na Tume ya Wakimbizi ya Umoja wa Mataifa kuhusu maombi yako ya ulinzi wa kimataifa.

10.6 Maelezo ya mawasiliano ya mashirika yaliyotajwa katika Muhtasari huu wa maelezo yako katika **Kiambatisho cha 1.**

**Ofisi ya Ulinzi wa Kimataifa**
**Huduma ya Uraia na Uhamiaji ya Ayalandi**
**Januari 2017**

## KIAMBATISHO CHA 1

## BAADHI YA MAELEZO YA MAWASILIANO

**International Protection Office**
Irish Naturalisation and Immigration Service,
79-83 Lower Mount Street,
Dublin 2. D02 ND99
Simu: 01 6028000
Faksi: 01 602 8122
Tovuti: www.ipo.gov.ie
Barua pepe: info@ipo.gov.ie

**International Protection Appeals Tribunal**
6/7 Hanover Street,
Dublin 2. D02 W320
Simu: 01 474 8400
Simu ya Bei nafuu: 1890 210 458
Faksi: 01 474 8410
Tovuti: www.protectionappeals.ie
Barua pepe: info@protectionappeals.ie

**Legal Aid Board**
Legal Aid Board Law Centre - Smithfield,
48/49 North Brunswick Street,
Georges Lane,
Dublin 7. D07 PE0C
Simu: 01 646 9600.
Tovuti: www.legalaidboard.ie
Barua pepe: lawcentresmithfield@legalaidboard.ie

**International Organisation for Migration.**
116 Lower Baggot Street,
Dublin 2. D02 R252
Simu ya bure: 1800 406 406
Simu: +353 1 676 0655
Tovuti: www.ireland.iom.int
Barua pepe: iomdublin@iom.int

**United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR)**
102 Pembroke Road,
Ballsbridge,
Dublin 4. D04 E7N6
Simu: 01 6314510
Barua pepe: iredu@unchr.org